**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM.**

**MAOMBI ANUAI NO. 400 YA 2022**

*(Yatokanayo na Tuzo ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi katika Mgogoro wa Kazi Na. CMA/DSM/UBG/007/21/008/21)*

**SHABANI SIGERA ....................................................MLETA MAOMBI 1**

**RASHIDI HAMISI ....................................................MLETA MAOMBI 2**

**MUSA KISAUTI ........................................................MLETA MAOMBI 3**

**SAIDINA KINANJA ..................................................MLETA MAOMBI 4**

**DHIDI YA**

**YIHAIKERRY-HYSEAS TRADING LIMITED.................MJIBU MAOMBI**

**UAMUZI**

**K.T.R MTEULE, J**

**30 Machi, 2023 & 28 Aprili, 2023**

Uamuzi huu unahusiana na pingamizi la awali lililoibuliwa na mjibu maombi akiwa na hoja mbili za kisheria. Katika hoja **ya kwanza** mjibu maombi anadai kwamba maombi haya hayawezi kusimama kisheria kutokana na kiapo kuwa na uthibitisho usiokuwa sawa kisheria. Katika **hoja ya pili,** mjibu maombi anadai kwamba maombi yanakiuka **Agizo la XIX Kanuni ya 3 ya Sheria ya Mwendendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33, ikirejewa 2019**.

Katika maombi haya, waleta maombi wanaomba muda wa nyongeza ili kuleta maombi ya marejeo dhidi ya tuzo ya Tume ya Usuluhishi na uamuzi Dar es Salaam, Ubungo (CMA) katika mgogoro wa kazi Na. CMA/DSM/UBG/007/21/008/21.

Katika majibu yake dhidi ya maombi haya, mjibu maombi amekuja na pingamizi la awali kama ilivyoelezwa hapo juu.

Pingamizi la awali lilisikilizwa kwa njia ya maandishi ambapo mjibu maombi amewakilishwa na **Wakili Langeni Robert Langeni** na mleta maombi amewakilishwa na **Wakili Hussein Hashim Msekwa**.

Akianza na hoja ya **kwanza** kuhusu kiapo kuwa na uthibitisho amba haupo sawa kisheria wakili Langeni Robert ana hoja kwamba waleta maombi wameshindwa kuweka usahihi wa aya ambazo wamezithibithisha katika kiapo jumuishi. Kwa mujibu wa wakili **Langeni Robert**, aya ambazo zinatakiwa kuwepo ni aya kumi na mbili (12) kwa ujumla wake lakini aya hizi hazijathibitishwa zote na waleta maombi na hivyo kufanya kiapo kukosa nguvu ya kusimama mbele ya mahakama hii, kwa kukiuka **Kanuni ya 3 ya Agizo XIX la Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai Sura 33,** ikirejewa 2019. Akirejea Agizo hilo, wakili **Langeni Robert** amewasilisha kwamba ni dhahiri unapowasilisha maombi yoyote mbele ya

mahakama inatakiwa kuzingati kanuni za uandikaji wa kiapo ili kiweze kukubalika, na kinyume chake, kiapo hicho kinakuwa hakina nguvu kisheria na kufanya maombi husika kutokuwa na umaana wowote mbele ya mahakama.

Akirejea nukuu ya **Agizo XIX la sura ya 33, na kifungu namba 53(2) cha Interpretation of laws Act,** wakili **Langeni Robert** amesema kuwa sheria imeweka ulazima kwa waapaji kuzingatia takwa la ni nini kiwekwe katika kiapo na hivyo haina budi matakwa hayo kufuatwa na kuzingatiwa. Alirejea maamuzi mbalimbali kuhusiana na hoja hii. Mojawapo ya kesi zilizorejewa ikiwa ni kesi ya **Easter Mwanjedsa vs DSW (Deutsche Stiftung Weltbevoelkerung), Revision Application No. 310 of 2019, High Court of Tanzania (Labour Division),** Dar es salaam.

Alitahadharisha kuwa kutokuzingatiwa kwa kanuni hizi hakuwezi kutibiwa na kanuni ya oksijeni (Oxygen Principles) kama ilivyosisitizwa kwenye kesi ya **Martin D. Kumalija & 117 Others v. Iron and Steel Ltd, Civil Application No. 70/18 of 2018, (unreported).**

Katika hoja ya pili ya pingamizi, Wakili **Langeni Robert** ameeleza kwamba, maombi haya hayakuzingatia matakwa ya kisheria kwa kuwa na kiapo chenye maneno ya kuambiwa (Hearsay) kinyume na takwa la

kisheria katika viapo na kushindwa kuzingatia **Agizo la XIX kanuni ya 3 ya sheria ya Mwenendo ya Mahauri ya Madai Sura 33, ikirejewa 2019**. Alieleza kuwa ukichunguza kiapo cha waleta maombi utaona kwamba waliofanya uthibitisho wa kiapo jumuishi ni watu wanne yaani Shabani Sigera, Rashidi Hamisi, Mussa Kisauti na Saidian Kinanja, wakati shauri namba 140 la mwaka 2022 ambalo lilifutwa mbele ya mahakama hii, Ndugu Mussa Kisauti ndiye pekee aliyekuwa anahudhuria kila siku shauri linapopangwa. Kwa maoni yake, kitendo cha kiapo cha waleta maombi kujumuishwa katika kiapo jumuishi na baadhi yao hawakuwa wanahudhuria katika shauri namba 140 of 2022, na kuthibiitisha katika sehemu ya uthibitisho wa kiapo kuwa yote waliyoyaelezea kwa aya kumi ni ya kweli na usahihi kwa ufahamu wao ni jambo ambalo halipo sawa katika kufuata kanuni za uandikaji wa kiapo.

Kwa maoni yake, pale mtoa kiapo anapotoa taarifa kutoka chanzo kingine basi anatakiwa kuelelzea katika sehemu ya uthibitisho wa kiapo kuwa taarifa hizo amezipata kutoka chanzo fulani, na kwa kushindwa kufuata kanuni hiyo katika uandikaji wa kiapo aya na maneno husika yaliyotolewa yanabaki kuwa maneno ya kuambiwa. Wakili **Langeni Robert** anapinga kitendo cha Shabani Sigera, Rashidi Hamisi na Saidiana Kinanja

kuthibitisha kuwa yote waliyoyaelelza kutoka aya ya kwanza hadi ya kumi ilihali walikuwa hawajawahi kufanya mahudhurio yoyote katika shauri namba 140 la 2022. Kwa maoni yake huu ni ukiukwaji wa matakwa ya **Agizo la XIX kanuni ya 3 ya sheria ya mwenendo ya mashauri ya madai Sura 33, ikirejewa 2019**.

Wakili **Langeni Robert** alikumbushia siku zilizopita kwamba waleta maombi waliwahi kuleta maombi kama hayo ambayo pia hayakuzingatia kanuni zilizowekwa kisheria, na kwamba hii ni mara ya pili jambo hili linafanywa tena na waleta maombi. Hivyo ameiomba mahakama kurejea maamuzi kadhaa yaliyowahi kuzungumzia kwa kina pale mleta maombi anapoleta maombi ambayo yana kasoro kisheria na jambo hilo likiwa linajirudia basi kesi au maombi hayo yanatakiwa kumalizika ili haki kutendeka.

Alirejea mojawapo ya kesi kuwa ni kesi ya **New Tabora Textile (T) Limited versus Tanzania Unioni of Industrial & Commercial Workers (TUICO), Revision no. 5 of 2016, High Court of Tanzania, Labour Division, At Tabora, (Unreported)**, ambapo Mheshimiwa Jaji L.L Mashaka, J. katika ukurasa wa 6 alirejea kesi ya **Stephen Masato vs Joseph Sinde Warioba & Attorney general, [1999] TLR 332** katika

ukurasa wa 342, na kusisitiza kuwa migogoro ni lazima ifikie mwisho na kwamba anayekuja kwenye haki ahakikishe ana mikono misafi kwa kutekeleza wajibu.

Wakili **Langeni Robert** aliiomba Mahakama kutupilia mbali maombi haya kwa kukosa uhalali kisheria.

Mawasilisho ya Waleta maombi yalifanywa na wakili Hussein Hashim Msekwa. Akijibu hoja ya kiapo kuwa na uthibitisho ambao haupo sawa kisheria kwa waleta maombi kutothibitisha aya zote zilizopo kwenye kiapo, alisema kuwa hoja za kiapo zina namba na namba hizo zimeorodheshwa kwenye uthibitisho. Kwa maoni yake, hakuna sehemu kwenye kiapo cha waleta maombi kumeandikwa aya na 11 na 12 kwa, hiyo hawawezi kuthibitisha aya ambazo hazipo kwenye kiapo.

Amepinga uhusiano wa kesi zilizorejewa na wakili wa Mjibu maombi na kiapo cha waleta maombi.

Kuhusu pingamizi la pili kwamba kiapo cha waleta maombi kuwa na maneno ya kuambiwa, **wakili Hussein Hashim Msekwa** alieleza kuwa pingamizi hili lina makosa mengi yanayotokana na kupindisha tafsiri ya sheria. Kwa maoni yake maombi yaliyopo mbele ya mahakama yanahusu nyongeza ya muda ili kuleta maombi ya marejeo ya Tuzo iliyotolewa na

Tume ya usuluhishi na Uamuzi (CMA). Alieleza kuwa kwenye Tuzo iliyotolewa na Tume waleta maombi walikuwa walalamikaji na walitoa ushahidi. Alihoji maneno ya kusikia yanatoka wapi wakati Tuzo inawahusu wao na maombi haya wameyaleta haohao.

Kwa maoni yake, hoja ya kuwa kwenye shauri na 140 la 2022 alikuwa anakuja Mussa Kisauti pekee na hivyo waleta maombi wengine wamesikia tu haina mashiko kwa sababu Shauri namba 140 la mwaka 2022 lilifutwa (struck out) na athari ya kesi kuwa "struck out" ni kwamba mwenendo wote wa kesi unafutwa inakuwa kama hakujawahi kuwa na kesi, na kwa sababu hii ndiyo maana waleta maombi wameleta maombi ya nyongeza ya muda.

**Wakili Hussein Hashim Msekwa** alisisitiza kuwa waleta maombi waliotajwa kwenye Hukumu ya mombi ya marejeo na 140 ya 2022 iliyotolewa na Jaji Mteule ndio hawahawa waliopo kwenye maombi haya. Alieleza pia kwamba Shauri Na. 140 linahusu maombi ya marejeo (REVISION), kwenye usikilizaji wa maombi ya Mrejeo hakuna ushahidi unaotolewa ila mahakama inapaitia maamuzi yaliyokwishatolewa. Kwa maoni yake, hata Mussa Kisauti asingefika bado kusingekuwa na tatizo

lolote kisheria kwa sabau waliajiri wakili na wakili anaruhusiwa kutoa hoja na kujibu kwa niaba ya wateja wake.

**Wakili Hussein Hashim Msekwa** alihitimisha kwa kuomba mapingamizi haya yatupiliwe mbali kwa sababu mjibu maombi ameshindwa kuonesha mapungufu yaliyopo kwenye maombi.

**Wakili Langeni Robert** aliwasilisha hoja jazilishi (rejoinder). Mawasilisho haya yatazingatiwa pia katika kuamua maombi haya.

Baada ya kupitia hoja za wadaawa, hoja kuu zipo mbili na nitazizungumzia moja baada ya nyingine. Nikianza na hoja ya kwanza kuwa aya za kiapo hazijathibitishwa zote, naona kuwa hakuna ubishi kuhusu suala la kisheria kuwa kutokuthibitisha hoja ni pungufu la kisheria linaloweza kusababisha kiapo kisiwe sahihi na kusimama kisheria. Hoja ya waleta maombi imejikita katika kutetea kuwa uthibitisho huo upo na hivyo hoja ya mjibu maombi haina mashiko.

Nimepitia kiapo cha waleta maombi nikabaini kuwa kuna hoja zimejirudia. Yaani kuna hoja mbili zimepewa namba 5 na hoja mbili zingine zimepewa namba 8. Ila ukiangalia uthibitisho wa waleta maombi, hoja hizi hazijatajwa kwa kurudiwa. Naona utata katika uthibitisho maana haijulikani ni numbe 5 ipi imethibitishwa na ni namba 8 ipi imethibitishwa katika zile zilizojirudia.

Hii ni dhahiri kuwa lipo tatizo katika uthibitisho kutokana na hoja zilizothibitishwa kutokuendana na mfumo wa kiapo ulivyojipanga. Kutokana na hali hii, nakubaliana na wakili wa mleta maombi kuwa kiapo kina kasoro na hivyo hakiwezi kusimama kisheria.

Hoja hii inatosha Mahakama kuona kuwa maombi haya hayawezi kuendelea kusimama kutokana na kiapo kutokuwa sawa. Hivyo sitalazimika kudadavua hoja ya pili kutokana na kile ninachoona kwamba hata ikionekana kuwa kuna pungufu la kisheria katika kuwepo kwa hoja za kuambiwa, bado amri ya mwisho itabaki kuwa ileile.

Nimezingatia hoja ya Wakili **Langeni Robert** kuwa kwa vile mapungufu ya kisheria yanajitokeza kwa mara ya pili, maombi haya yanastahili kutupiliwa mbali na siyo kuyaondoa. Natofautiana na wakili wa mjibu maombi kwa misingi ya haki inataka shauri limalizike kwa kusikilizwa kwa suala la msingi na siyo kwa masuala ya kiufundi. Hii ni kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kutoa fursa ya usikilizwaji wa shauri la msingi, ni vema wadaawa waliojikuta katika mapungufu ya kiufundi kupewa fursa ya kurekebisha mapungufu hayo. Kutokana na jambo hili, naona amri stahiki kwa shauri hili ni kuliondoa na kuwapa waleta maombi fursa ya kulifungua tena baada ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza badala

ya kutupilia mbali. Hivyo sikubaliani na hoja ya Wakili **Langeni Robert** kuwa maombi yatupiliwe mbali.

Kwa msingi huu basi, naona kuna hoja za msingi katika pingamizi la awali na hivyo maombi haya yanaondolewa na waleta maombi wanaruhusiwa kuyafungua tena yakiwa sahihi kisheria ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya uamuzi huu kama watapenda kuendelea na shauri. Hakuna amri kuhusu gharama.

Imeamriwa hivyo.

Imetolewa hapa Dar es Salaam leo tarehe 28 Aprili, 2023

**KATARINA REVOCATI MTEULE**

**JAJI**

**28/04/2023**